

SHAUKU YA MWALIMU MKUU: Maadhimisho ya *Mwezi wa Kitaifa wa Urithi wa Wahispania* Yastawi katika Shule ya Peachtree Middle

Katika Kaunti ya DeKalb, [Shule ya Peachtree Middle](#) imekuwa kitovu cha maadhimisho ya kufana na mfano mwema kwani matukio ya *Mwezi wa Kitaifa wa Urithi wa Wahispania* yameshuhudiwa kila mahali kwenye kumbi. Mwalimu Mkuu Michelle Perez, ambaye ana asili ya Hispania na Puerto Riko, amekuwa akiongoza maadhimisho haya ili kuunda mazingira ya kuvutia na jumuishi kwa wanafunzi wake wakati wa mwezi huu maalum wa utambuzi.

Mwezi wa Kitaifa wa Urithi wa Wahispania, unaoadhimishwa kila mwaka kuanzia tarehe 15 Septemba hadi 15 Oktoba nchini Marekani, ni wakati wa kuheshimu michango na ushawishi wa Wamarekani Wahispania kwenye historia, utamaduni na mafanikio ya taifa hili. Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb (DCSD) inajivunia takriban asilimia 20 ya wanafunzi wenye asili ya Hispania/Latino. Ingawa hiyo inapendeza, Shule ya Peachtree Middle ina asilimia 45 ya wanafunzi wake wa asili hii.

Mwalimu Mkuu Perez, ambaye ana shauku ya kukumbatia asili za wanafunzi wake, amechukua fursa hii kusherehekea maadhimisho haya ya kila mwaka ya urithi wa Wahispania pamoja na wanafunzi wake. Amekuwa akijihusisha kikamilifu na wazazi, akikuza majadiliano kuhusu asili yao ya Kihispania na nchi wanazotoka.

Mojawapo ya shughuli zinazotambulika katika Shule ya Peachtree Middle wakati wa *Mwezi wa Kitaifa wa Urithi wa Wahispania* ni shindano la kupamba milango ya darasa. Walimu na wanafunzi wanapamba milango yao kuwa maonyesho mahiri ya mapambo, historia na bendera kutoka nchi mbalimbali za Kihispania. Shule pia hujumuisha mafumbo wakati wa matangazo ya asubuhi na huchunguza mafanikio ya watu maarufu kutoka kwa jamii ya Wahispania.

“Imependeza kujifunza kutoka [milango ya mapambo] ninapotembea shuleni na kusoma kwenye milango watu tofauti ambao wamechagua kuangazia,” alisema Mwalimu Mkuu wa Shule Perez. “Tunawaambia ukweli ambao watoto wanapaswa kujadiliana katika madarasa yao, na kisha wanapiga simu kwenye ofisi ya mapokezi, kama ilivyo na simu ya redio, na tunawapa zawadi kwa kujua jibu.”

Zaidi ya maarifa wanayopata, masomo haya yanakuza mahusiano muhimu kati ya wanafunzi na walimu, na kupelekea mazungumzo kuhusu asili zao tofauti. Mwanafunzi wa gredi ya saba Brithany Avila pia alielezea furaha yake kwa kuwa na mwalimu mkuu wa asili ya Kihispania.

“Tuna mtu wa kuongea naye lugha ya Kihispania, kuzungumzia matatizo yetu yote na mtu anayetuelewa,” Brithany alisema. “Yeye ni mwalimu mkuu mzuri anayeelewa kila wakati hisia zetu. Anafanya shule iwe mahali pa furaha na vile vile pa kuelimisha.”

Wanafunzi wenzake Aviv Balsar na Michael Williams waliunga mkono maoni haya, wakisifu uongozi wa Mwalimu Mkuu wa Shule Perez na fursa wanazopata za kielimu.

“Ninapenda jinsi yeye si mbaya. Anajitahidi kuisaidia shule, hufanya kila mtu afurahie na kila mtu ahisi kuthaminiwa,” Michael alisema. “Nilijifunza mahali nchi ya Meksiko iko kwenye ramani na sifa zake nzuri, kama vile chakula kizuri.”

Aviv alikubali. “Sikujua mengi kuhusu urithi wa Wahispania, kwa hivyo imefurahisha sana kujifunza mambo mapya kuuhusu.”

Safari ya Mwalimu Mkuu wa Shule Perez kwenye uongozi katika Shule ya Peachtree Middle inatia moyo. Alianza kazi yake ya ualimu mwaka wa 2015 na, kupitia kujitolea kwake na athari yake, amepanda ngazi kwa utaratibu hadi juu. Safari yake ilifikia kilele alipoteuliwa kuwa mwalimu mkuu wa shule hiyo mnamo mwaka wa 2021, na kumfanya awe mwalimu mkuu wa DCSD akiwa na umri wa miaka 28 pekee.

Ingawa awali alipanga kuwa mwalimu, Mwalimu Mkuu wa Shule Perez alitumia kila fursa kuwatetea wanafunzi wake na kuleta mabadiliko kupitia jukumu hili kuu.

“Kila wakati huwa nawatania kwamba nilijipata kama mwalimu mkuu wa shule kibahati mbaya kwa sababu nimekuwa nikitaka tu kufundisha,” alisema Principal Perez. “Ninapenda sana kufundisha. Ni shauku yangu kuu, lakini mambo yakawa jinsi yalivyo. Ninapenda watoto na kuwatetea, na kila nafasi niliyopata iliniruhusu kufanya hivyo kwa kiwango kikubwa zaidi.”

Uongozi wa Mwalimu Mkuu wa Shule Perez umeleta athari kubwa kwenye Shule ya Peachtree Middle. Maono yake kwa mwaka huu wa masomo yamejikita kwenye usaidizi wa kimahusiano na kihisia wa wanafunzi, unaolenga kuhakikisha kwamba kila mwanafunzi anahisi kujaliwa, kuheshimiwa na kuthaminiwa.

“Hii inahusu kuzungumza na mwanafunzi yeyote shuleni na kumwuliza ikiwa anahisi kujaliwa,” alisisitiza. “Je, unahisi hapa ni mahali salama pa kusomea ambapo unaweza kujifunza bila kuhisi kuwa hujaliwi, hauheshimiwi au hauthaminiwi? Hii ndiyo imekuwa shauku kubwa mwaka huu.”

Ingawa *Mwezi wa Kitaifa wa Urithi wa Wahispania* unakaribia kumalizika rasmi kwa mwaka wa 2023, Mwalimu Mkuu wa Shule Perez anaahidi kuendelea kuwatia moyo wanafunzi na wafanyakazi wake, kuunda mazingira mazuri na jumuiishi ambapo uanuwai unakaribishwa na kila mwanafunzi anahisi kuthaminiwa.